**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**

# MIAKA 60 YA UHURU

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA SERIKALI KATIKA MANISPAA YA KINONDONI KUANZIA MWAKA 2000 ILIPOANZISHWA HADI 2020/2021



**Mhe. Songoro Mnyonge**
**Meya wa Manispaa**



**Hanifa Suleiman**
**Mkurugenzi wa Manispaa**

**Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania, Tanzania Imara, Kazi iendelee**

## 1. UTANGULIZI.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni moja kati ya Halmashauri tano za Mkoa wa Dar es Salaam inayoongoza kwa kuwa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanaoishi ndani ya Manispaa ikiwa ni pamoja na viongozi mbalimbali kutoka nje ya Nchi ya Tanzania. Imesheheni vivutio mbalimbali kutokana na Jiografia yake yenye mandhari nzuri, inayopakana na bahari ya Hindi upande wa Kaskazini ambapo kuna fukwe za bahari zinazofaa kwa shughuli za utalii na uvunaji wa rasilimali kama vile uvuvi wa samaki, majongoo bahari, chumvi na kadhalika.

Mbali na vivutio vya utalii na masuala ya uvuvi wa samaki na rasilimali nyingine Manispaa ya Kinondoni ni lango kuu la katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwa mikoa yote na Mataifa mbalimbali ikipakana na Wilaya za Bagamoyo iliyopo upande wa Magharibi mwa Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Ubungo na Wilaya ya Ilala Kusini Mashariki ambayo ni moja kati ya wilaya kubwa na zenye idadi kubwa ya watu kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Wilaya ya Kinondoni ni kati ya Wilaya zenye hali ya joto inayokadiriwa kuwa na nyuzi 35 katika miezi ya Januari hadi Machi. Hata hivyo joto hili hupungua hadi kufikia nyuzi 25 kwa miezi ya Juni hadi Agosti ambapo kiasi cha mvua hufikia wastani wa milimita 131.5 kwa mwaka. Kuna misimu miwili ya vuli mwezi Oktoba hadi Novemba na masika mwezi Machi hadi Mei kila mwaka.

Kwa mujibu Sensa ya watu nchini ya mwaka 1998 idadi ya watu katika Manispaa ya Kinondoni mwaka 2000 ilipoanzishwa kabla ya kugawanywa na Ubungo ilikuwa na watu 1,300,000 idadi inayokadiriwa kwa sasa kuwa ya wakazi wa Kinondoni pekee kutokana na Sensa ya Mwaka 2012. Idadi hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la watu wanaozaliwa na kuishi na uhamiaji kutoka nje ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna nyumba 343,391 zenye wastani wa watu 4 katika kila nyumba, Aidha katika kila kilometa ya eneo kuna watu 4,279 kwa sasa.

## 2. UTAWALA

Kiutawala Manispaa ya Kinondoni ina majimbo 2 ya Uchaguzi ya Kinondoni na Kawe, Tarafa mbili za Kinondoni na Kawe na Kata 20 na Mitaa 106. Baraza la Madiwani ni chombo cha juu cha Maamuzi likiundwa na wajumbe 34 ambapo 20 ni Madiwani wa kuchaguliwa kutoka katika Kata, 2 ni Wabunge wa kuchaguliwa katika Majimbo, 6 ni wa viti maalumu na 6 ni wa kuteuliwa na Rais. Aidha Kamati ya Maendeleo ya Kata ni chombo kingine cha maamuzi ngazi ya Kata ambacho ni kiunganishi cha Kamati ya Maendeleo ya Mtaa kama chombo cha maamuzi ngazi ya Mtaa.

Vyombo vyote hivi vinafanya kazi kwa pamoja na watumishi wa Manispaa katika ngazi husika ambapo kwa sasa kuna jumla ya watumishi 3,987 wa Kada mbalimbali katika ngazi zote.

**PICHA YA BARAZA LA MADIWANI**



## 3. UTEKELEZAJI HALISI WA ILANI YA UCHAGUZI

Ilani za uchaguzi za CCM kuanzia mwaka 2000 hadi sasa zime elekeza kuweka mpangilio mzuri wa shughuli za kiuchumi na huduma za kijamii kwa kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha huduma za kijamii. Katika Manispaa ya Kinondoni kumekuwa na mafanikio makubwa sana ukilinganisha miaka 60 iliyopita kutokana na kuelekeza msukumo zaidi katika kupiga vita umasikini, kuongeza mapato ya Serikali, mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi, kuimarisha mawasiliano, uboreshaji wa mazingira na maliasili, matumizi ya Sayansi na Teknolojia na kuimarisha, kupanua na kuboresha huduma za jamii hususani Elimu, Afya, Maji, Umeme, Masoko n,k. Hii imepelekea Manispaa yetu kufikia malengo yake na Nchi yetu kuingia katika uchumi wa kati.

Kimsingi kuna tofauti kubwa katika kasi ya utekelezaji halisi wa shughuli hizi katika kila sekta kulinganisha na miaka 60 iliyopita tukitathimini kuanzia mwaka 2000 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa rasmi na sasa kwa kuangalia huduma zinazoendelea kutolewa kwenye maeneo ya afya, usimamizi wa taka, miundombinu, maliasili, mazingira, biashara, maendeleo ya sekta isiyo rasmi, maendeleo ya miji, sheria, elimu, utamaduni, kilimo, ufugaji, maendeleo ya ushirika, maendeleo ya jamii na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

**PICHA YA JENGO LA MANISPAA**



## 4. MAPATO YALIYOKUSANYWA

Katika kipindi hicho Halmashauri ya Kinondoni imefanya jitihada kubwa katika ukusanyaji wa mapato, makusanyo ya ndani yameongezeka kutoka Tshs. 2,173,366,653 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa mwaka 2000 na kufikia Tshs. 100,408,608,175.65 zinazo kusanywa kwa sasa.

Kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, bajeti ya Manispaa ya Kinondoni ilikuwa Tshs. 107,114,781,500 kati ya fedha hizo Tshs. 59,951,312,000 ni fedha zilizotokana na Ruzuku kutoka Serikali kuu, Tshs. 42,170,304,000 ni Mapato ya ndani na Tsh. 2,296,986,195 kutokana na wadau mbalimbali. Hili ni ongezeko kubwa la bajeti ukilinganisha na bajeti ya Tshs. 2,173,366,653 kwa vyanzo vyote mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa.

Kuanzia mwezi Julai 2020 hadi kufikia Juni 2021 Manispaa ya Kinondoni imetumia Tshs. 95,594,049,789.84 katika utekelezaji wa kazi na shughuli mbalimbali za maendeleo. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na kiasi cha Tshs. 2,173,366,653 Kilichotumika katika mwaka 2000 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa. Ufanisi huu wa kiwango cha juu umetokana na jitihada, ubunifu na uaminifu wa watumishi wa Idara ya Fedha na kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki ambapo Manispaa ya Kinondoni ilikuwa Taasisi ya kwanza kuanza kutumia mifumo ikianza na mfumo wa Maxmalipo.

**PICHA YA MOJA YA VITUO VYA MAPATO**




## 5. SEKTA YA MIPANGO, URATIBU NA UFUATILIAJI

Manispaa ya Kinondoni inajivunia uwezo wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji inayofanya mambo makubwa katika kupanga, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogharamiwa na vyanzo mbalimbali. Uwezo wa kusimamia utekelezaji wa miradi umeongezeka kwa kuwa miradi inayosimiwa sasa ni yenye thamani kubwa ikipanda kutoka miradi yenye thamani ya Tshs. 400,000,000 mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa na kufikia miradi yenye thamani ya Tshs. bilioni 8.9.


Miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa kwa sasa chini ya Uratibu na Usimamizi wa Idara hii ni pamoja na ujenzi wa soko la kisasa Magomeni Tshs. 8,954,655,100, ujenzi wa soko la Tandale Tshs. 8,788,520,365, Ujenzi wa Kiwanda cha kuchakata taka na kuzalisha mbolea Tshs. 5,569,600,000, ujenzi wa ofisi ya Manispaa Tshs. 2,000,000,000, ujenzi wa Uwanja wa mpira Tshs. 4,500,000,000, ujenzi wa Kituo cha kisasa cha daladala Mwenge Tshs. 4,800,000,000, ujenzi wa jengo la ghorofa tatu katika Hospitali ya Wilaya Mabwepande Tshs. 1,899,997,704.40, ujenzi wa kituo cha Afya Bunju Tshs. 600,000,000, ujenzi wa Zahanati 2 katika Kata ya Magomeni na Makumbusho Tshs. 518,571,722, ujenzi wa madarasa 59 ya Sekondari Tshs. 939,431,927, ujenzi wa madarasa 46 ya shule za msingi Tshs. 900,000,000, na Ujenzi wa miradi ya UVIKO-19 inayoendelea kutekelezwa kwa mafanikio kwa sasa yenye thamani ya Tshs. bilioni 3.3.

**PICHA MRADI WA UVIKO-19**



**Shule ya Sekondari Kambangwa**

**PICHA YA ZAHANATI YA MAGOMENI**



## 6. SEKTA YA KILIMO UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika ya Manispaa ya Kinondoni yenye watumishi 20 wa Ugani ina jivunia mafanikio makubwa ya utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kutokana na uwepo wa rasilimali nyingi kwa ustawi na manufaa ya wananchi kama soko la mazao ya kilimo, watoa huduma binafsi wanaosaidia kupatikana kipato kwa wakulima, uwepo wa chakula katika masoko na Kituo cha kisasa cha Kilimo cha Malolo Kata ya Mabwepande.

**PICHA YA KITUO CHA KILIMO MALOLO**




Mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Manispaa ya Kinondoni katika sekta hii ya Kilimo mjini yametokana na kuelekeza huduma za ugani katika Kituo hiki cha Kilimo Malolo chenye eneo la eka 45 ambapo 75% zinatumika kwa maonesho na uzalishaji na 25% zinatumika kwa madhumuni ya ujenzi wa majengo ya utawala, maktaba, ofisi, maabara, ukumbi wa mafunzo na huduma nyingine zinazohusu utawala na uendeshaji.

Kwa sasa Kituo kina uwezo wa kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa watu 2050, kutoa mafunzo kwa vikundi 6 vya wakulima kuhusu uzalishaji, utunzaji fedha, utoaji taarifa za mwezi na usimamizi wa miradi. Aidha Manispaa imeanzisha chanzo chake cha maji kutoka mto Mpiji chenye uwezo wa kutoa lita 15,000 kwa siku zinazotumika katika kilimo cha umwagiliaji kinachofanywa katika hekta 100 na vikundi 18 vya wakulima wanaojengewa uwezo wa uzalishaji bora wa mazao ya kilimo kwa teknolojia ya kisasa kupitia Kituo hicho cha Malolo.

Huduma zinazotolewa katika kituo hiki ni pamoja na kanuni na mbinu za kilimo cha umwagiliaji, bustani za makontena, ulinzi wa mazao, kitalu nyumba, maandalizi na usimamizi wa vitalu vya mboga mboga na matunda, dhana za kilimo na ushauri kupitia mafunzo yanayotolewa kituoni hapo.

Kwa sasa ingawa Kilimo katika Manispaa ya Kinondoni kinachangia tani 466.74 tu za mazao ya chakula sawa na 0.18% tu ya mahitaji ya chakula kwa mwaka, ya tani 255,064.38, lakini hakuna upungufu wa chakula kwa sababu vyakula vingi hutoka nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Kimsingi dhima ya Manispaa ya Kinondoni ya kutoa huduma za ugani kwa njia ya matumizi sahihi ya rasilimali na yenye ufanisi na kuboresha shughuli za kilimo mijini imefikiwa kwani kuna uzalishaji wa tani 10-20 za mazao ya bustani kwa eka moja kutokana na teknolojia mpya inayotolewa na wataalamu wa nje kupitia ushirikiano wa Korea na wa ndani kupitia chuo cha Kilimo SUA.

**PICHA YA SHAMBA DARASA MALOLO**



## 7. SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Ubunifu na juhudi zinazofanywa na watumishi wa sekta hii katika kutoa huduma na kuboresha mazingira ya wafugaji na wavuvi umeifanya Manispaa ya Kinondoni kuwa moja kati ya Halmashauri tano za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zina machinjio ya kisasa na yenye mvuto. Hadi sasa Manispaa ya Kinondoni ina machinjio 15 kati ya hizo, machinjio 1 ni ya ng'ombe, 2 za nguruwe na 12 za kuku. Mwaka 2000 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa hakukuwa na machinjio hata moja ya kisasa. Aidha kwa sasa iko katika ukamilishaji wa ujenzi wa machinjio ya kuku katika masoko yake yote ya kisasa ya Kawe, Magomeni, Tandale na Tegeta Nyuki.

Vile vile kumekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa banda la kuku katika Kituo cha kilimo Malolo, ongezeko la makusanyo kutokana na machinjio kiasi cha Tshs. 177,196,144 na makusanyo yatokanayo na leseni za Uvuvi. Tshs. 96,378 kiasi ambacho hakikusanywa Manispaa ilipoanzishwa mwaka 2000.

**PICHA MACHINJIO YA KUKU SOKO LA KAWE**



Aidha katika kuimarisha na kuboresha huduma za mifugo na viwanda Manispaa ya Kinondoni imeweza kufanya ukaguzi mbalimbali kwenye sekta ya mifugo pamoja na vituo vya kutotoleshea vifaranga na mabucha ya nyama, kufanya maonesho ya Nane Nane na siku ya maadhimisho ya siku ya chakula duniani. Pia imeweza kutoa huduma ya tiba na kinga kwa wanyama ikiwa ni pamoja na kuhamasisha jamii umuhimu wa unywaji wa maziwa, kukusanya sampuli za vyakula sanjari na kutoa mafunzo ya umuhimu wa unywaji wa maziwa kwa binadamu.

## 8. SEKTA YA BIASHARA NA MASOKO

Hii ni moja ya sekta yenye mafanikio makubwa zaidi katika Manispaa ya Kinondoni kutokana na malengo na dhamira ya dhati ya manispaa katika kutatua kero za sekta hii na kilio cha muda mrefu kuhusu tatizo la maeneo rasmi ya kufanyia biashara yaani masoko. Serikali ya awamu ya tano na sita imetoa fedha nyingi kwa Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya kujenga masoko mawili ya kisasa ya Magomeni, Tshs. bilioni 8.9 na Tandale bilioni 7.8 ambapo Soko la Magomeni limekamilika na kuanza kutumika na Soko la Tandale litakamilika na kuanza kutumika Januari 2022.

Aidha Manispaa ya Kinondoni imejenga masoko yake mapya na kuyaboresha yaliyopo kwa fedha za mapato yake ya ndani. Masoko hayo ni pamoja na soko la Tegeta Nyuki, Africa sana, Msufini, Bunju na Makumbusho. Pia kuna soko la kisasa la Bwawani Kata ya Mwananyamala lililojengwa chini ya mradi wa DMDP na kufanya kuwa na jumla ya masoko bora 27 katika Manispaa idadi ambayo ni kubwa sana ukulinganisha na mwaka 2000 ilipoanziwa ikiwa na soko moja tu bora la Makumbusho.

**PICHA YA SOKO LA BWAWANI NA MAGOMENI**







Kukabiliana na upungufu wa maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara, Manispaa ya Kinondoni imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, imeweza kutenga maeneo ya wazi na fukwe zake na kuyaboresha hususani katika ufukwe wa Oysterbay maarufu Coco beach.

**PICHA YA MABANDA YA COCOBEACH**



## 9. SEKTA YA MIUNDOMBINU (UJENZI)

Sekta hii ni moja kati ya sekta muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa na wananchi. Ikumbukwe kuwa Tanzania tayari ilishaingia katika moja ya nchi zilizo katika uchumi wa kati ikichagizwa na kasi ya uboreshaji wa sekta ya miundombinu katika miaka ya hivi karibuni. Manispaa ya Kinondoni ni miongoni mwa Halmashauri zilizopiga hatua kubwa katika kuboresha miradi ya miundombinu ya barabara, madaraja, makalavati na mifereji ya maji ya mvua kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Manispaa kwa kushirikiana na TANROADS, TARURA na wadau wengine hususani wa miradi ya uboreshaji miundombinu ya Dar es Salaam (DMDP). Ni ukweli usiopingika kuwa sekta hii imepiga hatua kubwa sana ukilinganisha na mwaka 2000 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa.

**PICHA YA DARAJA**



Mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa kulikuwa na mtandao wa barabara zenye urefu wa Km 450 tu kati ya hizo Km. 125 tu zilikuwa za lami na Km. 325 zilikuwa za kiwango cha changarawe na vumbi. Kwa sasa mtandao wa barabara umefikia Km. 1,664.29 ambapo Km.163.968 ni za lami, Km. 635.98 ni za changarawe na Km. 864,342 ni za vumbi.

Mafanikio haya ya uboreshaji wa Sekta ya miundombinu kwa kujenga barabara, madaraja, makalavati na mifereji ya maji ya mvua na kuboresha miundombinu mingine kwa kiwango kikubwa yamesaidia kupunguza au kuondoa kabisa kero ya msongamano wa magari na mafuriko katika maeneo mbalimbali yaliyokuwa na changamoto na kero hiyo.

Aidha maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Kinondoni miundombinu yake imeboreshwa kwa kiwango cha kimataifa kupitia mradi ya DMDP kwa kujenga barabara za lami na zege, mifereji ya maji ya mvua, vivuko, makaravati, madaraja, njia za waenda kwa miguu na taa za barabarani hususani barabara ya TANESCO soko la samaki, barabara ya Makanya, barabara ya viwandani, barabara ya Kilongawima, barabara ya CDB – Makumbusho, barabara ya Uporoto, barabara ya

CCBRT na kadhalika. Pia kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa mto Ng`ombe kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi baharini.

**PICHA YA BARABARA YA DMDP**



Mafanikio haya ya katika sekta ya miundombinu yamerahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa kuwafikia haraka wananchi na kuwezesha ujasiriamali na biashara ndogo ndogo zinazo kua kwa kasi ukilinganisha na miaka 60 iliyopita.

## 10. ELIMU YA MSINGI

Serikali kupitia Halmashauri ya Kinondoni imefanya maboresho makubwa katika sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, ununuzi wa madawati, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo ya utawala na ukarabati wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa ofisi za walimu na ujenzi wa maktaba za shule za msingi.

Manispaa ina shule 165 za awali kati ya hizo 77 ni za Serikali na 88 za binafsi, shule za msingi 158 kati ya hizo shule 78 ni za Serikali na 80 ni za binafsi. Shule za Serikali zina wanafunzi awali na msingi 90,988 kati ya hao 45,527 ni wanaume na 45,461 wanawake. Idadi ya Walimu ni 1,863 kati yao Walimu 300 ni wanaume na Walimu 1,663 ni wanawake.

Aidha shule binafsi za msingi zina wanafunzi 34,240 kati ya hao wanaume ni 17,186 na wanawake 17,054. Zina jumla ya walimu 1,089 wanaume 755 na wanawake 334.

Moja ya mafanikio makubwa katika Sekta ya Elimu ni kupunguzwa kwa changamoto za upungufu wa madarasa, madawati, ofisi za walimu na maktaba zilizokuwa zinaikabili shule za Serikali. Kwa

sasa uwiano wa walimu na wanafunzi ni 1:50, uwiano wa madarasa na wanafunzi ni 1:76, uwiano wa madawati na wanafunzi ni 1:4 na uwiano wa matundu ya vyoo ni 1:16. Haya ni mafanikio makubwa ukilinganisha na mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa.

**PICHA YA MSINGI YA MIVUMONI**



## 11. ELIMU YA SEKONDARI

Katika kuhakikisha kuwa ufaulu wa wanafunzi unaongezeka katika shule za Sekondari kwa Manispaa ya Kinondoni, Manispaa kwa kushirikiana na Serikali kuu imeboresha zaidi sekta hiyo kwa kujenga shule mpya za Sekondari, kupandisha hadhi baadhi ya shule za Msingi na kuwa za Sekondari, kujenga mabweni, kununua madawati na kuondoa changamoto mbalimbali za kielimu zinazozikabili shule hizo.

Kwa sasa Manispaa ya Kinondoni ina shule 87 za Sekondari kati ya hizo 29 ni za Serikali na 58 ni za binafsi. Shule za Serikali zina wanafunzi 31,067 kati ya wanafunzi hao 14,907 ni wanaume, 16,160 ni wanawake. Zina jumla ya walimu 954 kati ya hao walimu 243 ni wanaume na walimu 711 ni wanawake.

Kama ilivyo kwa shule za msingi, mafanikio makubwa katika shule za sekondari yametokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Manispaa na Serikali kuu kuhakikisha kero na changamoto mbalimbali zimetatuliwa na kuwa na mazingira ya kuridhisha ya kutolea elimu.

Kwa sasa Uwiano wa madarasa kwa wanafunzi ni 1:60, uwiano wa madawati kwa wanafunzi ni 1:2, uwiano wa matundu ya vyoo ni 1:56. Aidha katika kutekeleza agizo la Serikali la kuhakikisha kila Kata inakuwa na Sekondari yake, Manispaa ya Kinondoni imejenga Sekondari katika Kata 19 kati ya Kata 20 za Manispaa na Kata nyingine zikiwa na Sekondari zaidi ya moja. Haya ni mafanikio makubwa ukilinganisha na mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa ambapo kulikuwa na Shule 2 tu za Sekondari za Wazazi na hivyo asilimia kubwa ya watoto walikosa elimu.

**PICHA YA SEKONDARI YA MZIMUNI**



Aidha mpango wa elimu bure katika shule za Msingi na Sekondari umechangia kuhamasisha wazazi na walezi kuwaendeleza watoto kielimu jambo ambalo limeonekana kuwa kichocheo kikubwa cha ufauli kwa wanafunzi kwa ufaulu umeongezeka sana ukulinganisha na mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa.

## 12. SEKTA YA USAFI NA MAZINGIRA

Manispaa ya Kinondoni kupitia Idara ya Usafi na Mazingira imeendelea kutekeleza kikamilifu na kwa mafanikio jukumu lake la kuratibu na kusimamia suala la ukusaji, uzoaji na usafirishaji wa taka hadi dampo likiwemo suala zima la kulipia gharama zake. Idara za Ujenzi, Afya na Mipangomiji zinatekeza sehemu ya majukumu hayo kwa kushirikiana na Idara ya Usafishaji na Mazingira.

Kwa sasa Manispaa inazalisha tani 1,223.6 Kwa siku, sawa na tani 446,614 kwa mwaka. Uwezo wa kuzikusanya ni tani 773.3 kwa siku sawa na tani 278,388 kwa mwaka sawa na asilimia 63.2 kwa siku. Aidha taka zote zinazokusanywa husafirishwa kwenda dampo umbali wa Km. 35 ambapo hulazimika kusafiri umbali wa Km. 70 kwa tripu moja na kufanya kuwa moja ya changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Idara hiyo.

**PICHA YA MAGARI YA TAKA**



Pamoja na changamoto hiyo kumekuwa na mafanikio makubwa ukilinganisha na mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa kwani uwezo wa kuzalisha taka ulikuwa chini ya tani zinazozalishwa sasa kwa siku na uwezo wa kuzikusanya na kuzisafirisha hadi dampo ulikuwa chini ya uwezo wa sasa ambapo zilikuwa zikikusanya na kusafirishwa kwa kutumia teknolojia duni ukilinganisha na sasa kuna matumizi ya mashine za kisasa ambapo Manispaa ina tipa 2, skipu loda 5, trekta 1, matela 10 na mashine nyingine katika Kiwanda cha kuchakata taka Mabwepande.

Uwepo wa Kiwanda hiki cha kisasa cha kuchakata mbolea ya Mboji inayotokana na taka za Masokoni kitakachochakata tani 50 kwa siku na kuzalisha tani 25 za mboji kwa siku, pamoja na kuongeza mapato ya Manispaa kwa kuuza mbolea inayozalishwa, kitapunguza gharana za kukusa na kusafirisha taka za Masokoni kwenda dampo na kutoa ajira kwa Wananchi.

Mafanikio mengine makubwa katika Sekta hii ni ushiki wa wadau muhimu wa taka kama Serikali Kuu, Manispaa, vikundi vya kijamii kama NGO na CBO na wafadhili wengine jambo ambalo halikuwepo katika miaka 60 iliyopita na mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa kwani lilikuwa ni jukumu la Halmashauri pekee jambo lililopelekea kuwa na ufanisi duni.

**PICHA YA KIWANDA CHA MBOLEA**




## 13. SEKTA YA AFYA

Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Afya katika Manispaa ya Kinondoni yametokana na Ushirikiano mkubwa katika jukumu la kutoa huduma za Afya. Pamoja na ukweli kuwa ni jukumu la Manispaa kutoa huduma za Afya, ushirikiano wa wadau na jamii ikiwemo Serikali kuu, Sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Kimataifa umekuwa na mchango mkubwa katika Mafanikio ya Sekta hii.

Kwa sasa Manispaa ina Vituo 317 vya kutolea huduma za Afya. Kati ya hivyo 28 ni vya Serikali na 289 ni vya binafsi. Manispaa kupitia idara ya Afya imepiga hatua kubwa sana katika utekelezaji wa jukumu la kuhakisha wakazi wote wa Manispaa ya Kinondoni wanafikiwa na huduma za Afya kwa kujenga Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati katika Kata mbalimbali ambapo kata 19 kati ya kata 20 za Manispaa zina huduma hizo na Kata 1 tu ya Kinondoni inatarajiwa kupata huduma hiyo katika mwaka huu wa fedha. Pia Hospitali ya Wilaya Mabwepande iko katika hatua za mwisho kukamilika na imeanza kufanya kazi.

**PICHA YA HOSPITALI YA WILAYA MABWEPANDE**



Viashiria mbalimali vinaonyesha kuwa jitihada hizi zimekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali ya Afya na ustawi wa Watu kama, Kupungu kwa vifo vya watoto, Watoto chini ya miaka 5 na Wajawazito,Kuongezeka kwa umri wa kuishi,uhakika wa maji safi na salama, idadi ya watu wanaofikiwa na huduma za Afya,kipato cha wananchi kwa siku, kiwango cha kuondoa ujinga,uwiano mgonjwa kwa Daktari, wagonjwa na wakunga, wagonjwa na nafasi ya vitanda na ukaribu wa upatikaji wa huduma hizo kwa Wananchi.

Kiwango cha vifo vya watoto kwa sasa ni 2/100, vifo vya watoto chini ya miaka mitano ni 2/1000, muda wa kuishi ni miaka 60 kwa wanaume na miaka 61 kwa wanawake, vifo vya wajawazito ni 66/100,000, vifo vya watoto wanaozaliwa chini siku 28**{**Neomaal mortality rate [NMR]} ni 7.0/100, uhakika wa upatikanaji wa maji safi na salama ni 85%, kiwango cha ujinga ni 58%, ukaribu wa huduma za Afya {facility within radius of 5Km. ni 80%, watu wenye uhakika wa vyoo bora ni 85%, kipato cha mwananchi kwa siku ni $76.8,uwino wa wagonjwa na wakunga ni 1:3579, uwiano wa wagonjwa na Daktari ni 1:100, uwiano wa wagonjwa na vituo vya kutolea huduma ni 1:7285, kiwango cha uzazi{TFR} ni 5.4%, ongezeko la watu ni 4.1%, crude Death rate ni 248/1000, uwiano wa wagonjwa na vitanda ni 1:1.18 na nafasi ya kitanda ni 109.

Aidha licha ya uwepo wa ugonjwa hatari wa Corona na Virusi vya UVIKO -19 Manispaa imefanya jitihada kubwa kutoa elimu juu ya uwepo wa ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo. Katika kutekeleza hilo jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na Kuweka vitakasa mikono katika maeneo yote ya mikusanyiko ya watu, kuwahimiza wananchi kuvaa barakoa kila wanapokuwa katika mikusanyiko na kuwapa chanjo ya UVICO 19.

**PICHA YA KITUO CHA AFYA KIGOGO**



Mafanikio yote haya yametokana na jitihada za serikali ya awamu ya sita kuendeleza mipango na mikakati ya Serikali ya awamu ya tano sambamba na ushirikishaji wa jamii kupitia bodi ya Afya ya Manispaa na Kamati za vituo vya kutolea huduma katika ngazi zote kwa kuhakikisha watu wote wanapata huduma bora zinazowezekana na uangalizi mzuri. Pia kumekuwa na ushirikiano mkubwa na NGOs, FBOs, CBOs na Waganga wa Tiba mbadala. Pia kuna mchango Taasisi na Mashirika ya Kimataifa kama Pathfinder, CCBRT, MDH, PST, Medipeace, JHPIEGO na APHTA.

Sekta nyingine za umma ndani ya Manispaa ya Kinondoni kama elimu, afya, maji, ujenzi maendeleo ya jamii, kilimo na mifugo pia zinajishughulisha katika kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo ukaguzi na usimamizi.

## 14. SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Sekta ya maendeleo ya jamii ndiyo sekta ambayo inaigusa jamii yenye kipato cha chini hivyo Serikali kwa kulitambua hilo iliweka mpango mkakati wa kuweza kutoa mikopo isiyo na riba kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ili kuchochea wananchi kuanzisha ujasiriamali mdogo na kuinua kipato chao na hivyo kuchangia katika pato la Taifa. Kwa sasa uwezeshaji wa Manispaa ya Kinondoni kupitia mikopo hii kwa wanawake vijana na watu wenye ulemavu umeongezeka kutoka Tshs. milioni 400 kwa mwaka ilipoanzishwa mwaka 2000 hadi Tshs. bilioni 5.2 kwa mwaka. Mfano hadi kufikia Julai, 2021 imetolewa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu yenye thamani ya Tshs. 8,669,125,350 na marejesho ya Tshs. 5,323,400,084.39 ambapo vikundi 3,510 vya Wanawake vimekopeshwa Tshs. 3,424.206,100, vikundi 1,866 vya Vijana vimekopeshwa Tshs. 2,358,650,250 na vikundi 43 vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa Tshs. 77,100,000.

**PICHA YA UTOAJI MIKOPO**




Moja ya majukumu ya sekta hii ni kushughulikia masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake, watoto, vijana na wazee ambapo kwa mafanikio makubwa Idara imesimamia utekelezaji wa Sera ya maendeleo ya jamii, maendeleo ya mtoto, maendeleo ya jinsia, kupunguza umaskini na Sera ya Taifa ya UKIMWI. Hii ni pamoja na kuijengea jamii uelewa wa fursa na vikwazo kwa maendeleo, kuihamasisha jamii matumizi bora ya rasilimali sambamba na kuishirikisha na kuiunganisha jamii kuanzia vikundi vidogo vidogo hadi jamii kubwa.

## 15. SEKTA YA MAENDELEO YA MIJI

Kujengeka vizuri kwa Miji duniani ni pamoja na uwepo wa mpangilio mzuri wa sekta ya Mipangomiji jambo ambalo Manispaa ya Kinondoni imejidhatiti kuhakikisha wanachi wake wanaishi katika mpangilio unaotakiwa na unao wezesha upatikanaji wa huduma zote muhimu na kazifikia kwa urahisi.

Kabla ya Uhuru na baada ya Uhuru hususani mwaka 2000 Manispaa ya Kinondoni ilipoanzishwa kulikuwa na changamoto kubwa ya uwiano wa ukuaji wa mji na maedeleo ya miundombinu na huduma nyingine za kijamii kwani kasi ya ukuaji na kupanuka kwa miji na ongezeko la watu ilikuwa kubwa kuliko kasi ya upangaji, upimaji na undaaji wa viwanja kwa ajili ya makazi na huduma nyingine za kijamii kutokana na tatizo la maendelezo yasiyoratibika.

Hii ilisababisha changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi holela, maeneo mengi kutofikika kirahisi, ubovu wa miundombinu, mafuriko, uhaba wa huduma za kijamii kama maji safi na salama, barabara na makazi bora na tofauti ya kimaendeleo na huduma za kijamii kati ya eneo moja na jingine ikiwemo ugumu katika kuboresha huduma za zamani za kijamii na kuzipanua katika maeneo hayo.

Manispaa ya Kinondoni imeendelea kukabiliana na changomoto zote hizi kwa kutumia njia ya kisasa ya upangaji kuanzia chini na kushirikisha wadau wote muhimu wa ardhi njia ambayo inayozingatia mahitaji ya jamii ikiwemo sekta rasmi, sekta isiyo rasmi na sekta binafsi na kuondokana kabisa na upangaji wa kizamani ambao ulianzia juu na haukushirisha wadau wote na kusababisha kero na matatizo mbalimbali.

Kwa kutumia mfumo wa EPM kama njia mpya ya upangaji umewezesha kufikia malengo yalikusudiwa kwa wakati. Kazi mbalimbali kama utatuzi wa migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na upimaji wa viwanja, urasimishaji wa makazi na ujenzi wa jengo la Ofisi za mradi wa ILMS katika Manispaa ya Kinondoni zimefanyika. Hii imewezesha upangaji na usimamizi wa kisasa wa ardhi kwa njia ya mifumo ya kompyuta {Computer Urban Management Information System {CUMT}.

Mafanikio mengi yamepatikana ikiwa ni pamoja na kupungua kwa ujenzi holela ulioachwa bila kudhibitika na kupelekea uharibifu wa miundombinu kama vile maji, barabara na kadhalika.

Kupungua kwa tatizo la uvamizi wa maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa shughuli maalumu kama vile Zahanati, Shule na Viwanja vya Serikali na kuboreshwa kwa maeneo mengi yalikuwa na changamoto ya mafuriko kwa kuwezeshwa kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua kama Mwananyamala, Kijitonyama, Tandale, Hanasifu, Msasani, Kinondoni, Magomeni, Mzimuni, Kigogo n.k.

## 16. MIRADI YA KIMKAKATI

Uanzishwaji wa Miradi ya Kimkakati ni moja ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kuu ili kuongeza mapato na kuinua uchumi sambamba na uboreshaji wa miundombinu yenye malengo hayo. Katika kutekeleza hili Serikali kuu imetoa jumla ya Tshs. bilioni 16.7 kwa Manispaa ya Kinondoni kuanzisha na kutekeleza miradi ya kimkakati ambapo Tshs. bilioni 8.9 zimetumika kujenga soko la Magomeni na Tshs. bilioni 7.8 zimetumika kujenga soko la Tandale.

Katika kuunga mkono jitihada za Serikali kuu Manispaa ya Kinondoni imeanzisha miradi yake ya Kimkakati ya kuongeza ukusanyaji wa mapato yake ya ndani pamoja na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Manispaa. Katika kufikia lengo hilo Manispaa ya Kinondoni imewekeza katika miradi mingine ya ujenzi wa stendi ya Mwenge, ujenzi wa Uwanja wa Mpira na uboreshaji wa Fukwe.

Soko la kisasa la Magomeni ni miongoni mwa Masoko bora kabisa nchini ambalo limegharimu kiasi cha Tshs. 8,954,655,000 soko la Tandale Tshs. 8,788,520,365 na soko la Bwawani lililojengwa chini ya mradi wa DMDP limegharimu Tshs. 1,020,000,000. Aidha miradi mingine ya

kimkakati ni ya uwekezaji iliyobuniwa na kutekelezwa na Manispaa ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa uwanja wa Mpira wa miguu Mwenge kwa Tshs. 4,500,000,000, ujenzi wa Stendi ya mabasi ya Mwenge kwa Tshs. 4,800,000,000, na miradi mingine ya Uwekezaji kwa ubia kama Oysterbay villa, Makumbusho na Texas ambayo inaongeza uimarishwaji wa sekta nyingine kwa mapato makubwa yanayopatikana kutokana na miradi hiyo.

**PICHA YA JENGO LA UWEKEZAJI OYSTERBAY VILLA**



## 17. SEKTA YA MAJI

Zaidi ya 81% ya wakazi wa Manispaa ya Kinondoni wanauhakika wa kupata maji safi na salama yakitoka Ruvu juu na Ruvu chini vyanzo vinavyosimamiwa na DAWASA. Chanzo hiki ni sawa na 81% ya maji yanayotumika katika wilaya ya Kinondoni na 19% inayobaki ni maji ya visima virefu na vifupi vinavyomilikiwa na umma na watu binafsi.

Kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa mwaka 1995 hakukuwepo na visima vilivyochibwa katika Manispaa ya Kinondoni hivyo maji ya bomba pekee yalikuwa yakitumika. Mwaka 2000 Manispaa ilipoanzishwa Tshs. 147,000,000 tu zilitumika kuchimba visima vifupi 21 katika maeneo mbalimbali ambapo kiasi cha shilingi Tshs. 340,000,000 zilitumika kuchimba visima virefu 34 katika maeneo mbalimbali. Aidha, kwa sasa Manispaa ina vyanzo vyake vingi vya maji hususani mto Mpiji kinachozalisha lita 15,000 kwa siku zinazotumika kwa kilimo cha umwagiliaji.

Uthibitisho kuwa sekta ya maji imeboreshwa kwa kiwango kikubwa unatokana na ukweli kuwa imefikia lengo na takwa la Sera ya maji kwa kuwezesha 81% ya wakazi wake kupata maji safi na salama chini ya umbali wa mita 400.

**MRADI WA MAJI MAKONGO**



## 18. SEKTA YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Kuinua, kuimarisha na kuendeleza sekta ya utamaduni na michezo ni moja ya kipaumbele kilichotekelezwa na Manispaa ya Kinondoni ambapo imesimamia kikamilifu utekelezaji wa sera sheria, kanuni na taratibu kuhusu sanaa na michezo kama kusajili na kutoa vibali vya sanaa ambapo kuna vikundi 389 vya sanaa kumbi 295 za burudani na watengenezaji wa filamu 98.

Kwa upande wa klabu za michezo zimesajiliwa klabu 256 za mpira wa miguu ikimo KMC FC iliyofanikiwa kushiriki mashindani ya kimataifa katika Shirikisho Barani Afrika mwaka 2019 na sasa inafanya vizuri katika ligi kuu.

**PICHA YA TIMU YA KMC FC**



## 19. MWISHO

Katika kuendeleza mafanikio ya kipindi kijacho, Manispaa ya Kinondoni imejiwekea vipaumbele vya jumla ambapo katika mwaka huu wa Fedha 2021/2022 vipaumbele vyake ni pamoja na kuimarisha mapato ya ndani kwa kuanzisha miradi ya kimkakati ya Tshs. bilioni 9.3, kuimarisha usafi na mazingira Tshs. bilioni 5.6, kujenga uwezo kwa jamii Tshs. bilioni 3.9, kuboresha utoaji wa huduma za elimu kwa kujenga na kuboresha miundombinu katika shule za msingi na Sekondari Tshs. bilioni 3.4, kuboresha utoaji wa huduma za afya Tshs. bilioni 2 na ulipaji fidia ya maeneo ya miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali Tshs. bilioni 1.